

## Tunakupa usaidizi

*Platform against Human Trafficking*

ina mpango maalum wa usaidizi ambao utakusaidia, hata jamii inapokosa kufanya hivyo. Pia tunapokea watoto ndani ya mpango. Usaidizi wetu ni wa bila malipo na usio na masharti – iwe unaishi Uswidi bila stakabadhi au hutaki kushirikiana na polisi. Usaidizi wetu unategemea mahitaji yako na uwezo wetu – bila kuhusisha mamlaka ikiwa hutaki kufanya hivyo.



PLATTFORMEN  
MOT MÄNNISKOHANDEL

## Unahitaji usaidizi au taafira zaidi?

Wasiliana na *The platform against human trafficking* kupitia tovuti yetu

[www.manniskohandel.se](http://www.manniskohandel.se)

Anwani ya barua pepe ni [info@manniskohandel.se](mailto:info@manniskohandel.se)

**KUMBUKA! Endapo kuna dharura, wasiliana na polisi kwa nambari ya simu 112.**

*National Secretariat Against Prostitution na Human Trafficking* zinaweza kuipa ushauri na taarifa mamlaka, manispaa na NGO zinazokutana na watu walio hatarini. Piga simu **Simu ya Dharura 020-390 000.**

MFUMO WA KUPINGA BIASHARA  
HARAMU YA BINADAMU

## TUNAKUPA NJIA MBADALA

**Binadamu wote wana haki ya maisha ya hadhi, yasiyo ya kushurutisha na kudhibiti.**

- **Ikiwa huwezi** kukubaliana kuhusu masharti ya kufanya kazi, hupati malipo na huwezi kuacha kazi na kuondoka.
- **Usipofanya hivyo** una uhuru wa kushawishi maisha yako binafsi au kuamua kuhusu mwili wako binafsi.

**Hiyo si Sawa!**

Inaweza kuwa biashara haramu ya binadamu.

SWAHILI

## Hii ni biashara haramu ya binadamu.

Unalazimishwa au kuhadaiwa kuuza ngono, kufanya kazi bila malipo, kuiba au kutekeleza uhalifu mwingine au kuomba? Hiyo ni biashara haramu ya binadamu. Si Sawa. Kila mtu ana haki ya kuishi kwa uhuru.

Hakuna aliye na haki ya kuwachochea wengine kutenda mambo kwa manufaa, raha au tamaa yao. Mtu anayemfanya mwingine kutenda haya anakiuka sheria ya Uswidi na haki za binadamu.



## Haki zako ni zipi?

Una haki ya kupata usaidizi ikiwa utahusishwa katika biashara haramu ya binadamu.

Una haki ya kupata:

- ✓ Chumba cha kinachofaa na salama
- ✓ Usaidizi wa nyenzo (chakula na mavazi, n.k)
- ✓ Huduma ya matibabu inayohitajika
- ✓ Usaidizi wa kisaikolojia
- ✓ Ushauri na taarifa za kisheria
- ✓ Tafsiri na ukalimani

Lengo letu ni kukuwezesha kupata haki hizi za binadamu. Sisi tunaoshughulikia mambo haya, tunafanya kazi pamoja katika shirika *The Platform against Human Trafficking*. Kwa pamoja tunataka kukupa wewe na watoto na familia yako usaidizi na ulinzi. Usaidizi wote ni wa bila malipo na kulingana na mahitaji yako.

## Baadhi yao waliosaidiwa:

*Evelina wa Bulgaria alilazimishwa kufanya kazi kila siku ya wiki bila fidia. Alikuwa akitafuta kituo cha usaidizi ili kujiondoa kwenye hali yake. Alisaidiwa kupata eneo salama la kukaa, chakula, kupumzika na mavazi. Alipokea taarifa kuhusu haki zake na nafasi mbadala.*

*Nadja wa Romania aligunduliwa na polisi ilipokuwa ikiwatafuta wanunuzi wa ngono. Nadja aliwekwa kwenye chumba ambapo alisaidiwa kupata nafuu baada ya kunyanyaswa katika ukahaba. Watoto wake pia walisaidia kutambua walichokuwa wamekiona na kushuhudia na Nadja alisaidiwa kuwasilisha ripoti ya polisi.*

*Anxa alikamatwa na kupewa dawa na kundi vamizi liliomlazimisha kuingia kwenye ukahaba. Alipokuwa mjamzito, alitorokea Uswidi na mtoto wake wa kiume wa umri wa miaka 3. Kupitia mpango wa usaidizi wa Platform, alipokea makao, ushauri, taarifa, mavazi, chakula na usaidizi kwa mchakato wa hifadhi.*